*Kioo cha Lugha* **2, 1996/97:61-70**

# Maana na Matumizi ya Upambanyaji: Tahakiki ya *Rosa Mistika*

*Mwenda Mbatiah*[*]

## 1. Utangulizi

Katika taaluma ya fasihi kufikia sasa, kuna nadharia chungu nzima ambazo zinatumiwa kama misingi na miongozo ya kuhakikia kazi za kifasihi. Nadharia kimekuwa kipengele muhimu katika ufundishaji wa fasihi hivi kwamba katika vyuo vikuu vingi kote ulimwenguni kipengele hiki kinafundishwa kama kozi huru inayochukuliwa kuwa yenye umuhimu mkubwa. Utafiti, uhakiki na ufundishaji wa fasihi barani Afrika hauwezi kuepukana na mkondo huu. Tatizo lililopo ni kwamba takriban nadharia zote zinazotumiwa wakati huu ni za kigeni. Hivi ni kusema kuwa asili yake ni nje ya bara la Afrika. Ni nadharia ambazo zimeibuka kutokana na mazingira mahususi ya kijamii na kihistoria ya mataifa ya Ulaya na Marekani. Katika manzili haya, swali linalozuka ni kwamba je, nadharia hizo za kigeni zinafaa kuhakikia fasihi za Kiafrika? Hili ni swali ambalo linaendelea kuchemsha bongo za wanafasihi wengi. Kumezuka mitazamo na mielekeo inayotofautiana kuhusu suala hili. Kuna wale wanaoonelea kwamba Waafrika wenyewe wanapaswa kubuni nadharia itakayofaa kuhakikia fasihi za Kiafrika. Tapo hili linachukulia kwamba uhakiki wa fasihi za Kiafrika unapotoshwa na matumizi ya nadharia za kigeni. Mwelekeo huu unawakilishwa na watu kama Chinweizu, Jemie na Madubuike katika kitabu chao: *Toward the Decolonization of African Literature* (1985).

Pia kuna wanafasihi wa Kiafrika wanaochukulia kwamba nadharia za kigeni zikifanyiwa marekebisho fulani zitafaa kuhakikia fasihi za Kiafrika. Marekebisho kama hayo ni kwa mfano kuoanisha vipengele vya nadharia (za kigeni) mbili au zaidi. Hivyo ndivyo alivyofanya Sunday Anozie.[1] Amejaribu kuoanisha taratibu za kisosholojia na zile za umuundo. Mwelekeo wa tatu ni ule unaochukulia kwamba mhakiki wa Kiafrika akiwa mwangalifu kuteua nadharia ifaayo katika mazingira yake, atapata mwongozo bora wa kuhakikia fasihi ya jamii yake. Ni katika mwelekeo

[*] Mhadhiri, Idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Nairobi

kama huu ambapo wahakiki wengi wa Kiafrika wametumia nadharia ya Umaksi wanayoona kuwa inafaa katika mazingira ya Kiafrika. Kwa kweli Umaksi umekuwa na athari kubwa sana katika taaluma ya fasihi barani Afrika. Fasihi ya Kiswahili haijaepuka athari kubwa ya nadharia hii.

Dhamira ya makala hii sio kuendeleza mjadala juu ya nadharia ifaayo katika uhakiki wa fasihi za Kiafrika. Tunakubali kwamba mjadala huu ni muhimu na unafaa kuendelea. Hata hivyo tunaonelea kwamba kwa sasa ni muhimu kwa msomi anayejishughulisha na fasihi hasa ya Kiswahili—kuzifahamu vizuri na kuweza kuzitumia nadharia za kisasa za uhakiki. Kutokuwepo kwa nadharia yenye asili ya Kiafrika (au ya kigeni) inayoafikiwa na wanafasihi wote wa Kiafrika hakumpi mhakiki wa fasihi ya iswahili udhuru wa kutozifahamu nadharia za kisasa zinazotumiwa kote ulimwenguni. Kila mojawapo ya nadharia hizo ina matatizo yake na inafaa kutumiwa kwa uangalifu hasa kuhakikia fasihi za Kiafrika katika lugha za Kiafrika kama Kiswahili.

Hoja zilizotolewa hapo juu ndizo zilizonipa ghera ya kushughulikia upambanyaji—ambayo ni mojawapo ya nadharia za kisasa za uhakiki. Kufikia sasa nadharia hii haijaota mizizi katika uhakiki wa fasihi ya Kiswahili. Katika makala hii tutaifafanua nadharia yenyewe, kasha tutaitumia kuhakikia riwaya ya Kezilahabi: *Rosa Mistika*. Hatukuichagua riwaya hii kwa sababu yoyote maalum, bali kwa kuchukulia kwamba inafahamika na watu wengi ambao wanatarajiwa kusoma makala hii.

Kwa kuwa upambanyaji bado ni nadharia ngeni katika uhakiki wa fasihi ya Kiswahili kwa Kiswahili jamii inayohusika na uhakiki wa fasihi hii haijakaa na kukubaliana juu ya tafsiri muafaka za dhana na istilahi za nadharia hii. Kwa kweli hili ni tatizo linaloikabili taaluma nzima ya uhakiki wa fasihi ya Kiswahili kwa Kiswahili. Ufafanuzi wa upambanyaji katika makala hii utafanywa kwa kutumia istilahi zilizozoeleka miongoni mwa wahadhiri wa fasihi ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

## 2. Ufafanuzi wa Upambanyaji

Mojawapo ya sifa za nadharia za kisasa za fasihi ni jinsi zinavyoingiliana. Kinachosababisha hali hii ni kwamba baadhi ya nadharia hizo zimetokana au zimeundwa kutokana na nadharia nyingine. Baadhi ya nadharia zinazoingiliana na hivyo kufanana katika vipengele vingi ni kwa mfano, umuundo, urasimu (au urasimu wa Kirusi) na uhakiki mpya. Umuundo ulijengeka katika msingi uliowekwa na urasimu. Kwa kweli kuna wanafasihi

wanaochukulia kuwa uhakiki mpya ni sura nyingine ya urasimu. upambanyaji nao unahusiana na umuundo, kama tutakavyoona baadaye. Kwa kiasi kikubwa chimbuko la nadharia zote zilizotajwa hapo juu ni mawazo ya mwanaisimu wa Kiswizi anayejulikana kama Ferdinand de Saussure (1857–1913). Hatuna nafasi ya kufafanua kikamilifu mawazo ya mtaalamu huyu katika makala hii. Tutagusia tu vipengele vya mawazo yake ambavyo vitasahilisha ufafanuzi wa nadharia ya uumbuaji.

Saussure alisema kuwa lugha ni mfumo uliojengeka kutokana na alama ambazo ni unasibu na ulinganuzi. Alama alizomaanisha Saussure ni maneno. Alama, kwa mujibu wa Saussure, ina sehemu mbili, ambazo ni umbo na dhana au maana. Umbo ni kiashiria na maana ni kiashiriwa. Neno "mbwa" kwa mfano, ni umbo/kiashiria ambalo linarejelea dhana/kiashiriwa ya mnyama anayefugwa katika muktadha wa lugha ya Kiswahili. Kwa mujibu wa Saussure, alama zina sifa mahsusi ambazo zinauwezesha mfumo wa mawasiliano wa lugha kufanya kazi. Zifuatazo ni baadhi ya sifa muhimu za alama:

(a) *Unasibu:* Uhusiano baina ya elementi za alama ni wa kinasibu. Tukiurejelea mfano wetu wa "mbwa", tunachomaanisha ni kwamba hakuna uhusiano wa kimantiki baina ya neon hilo na dhana ya mnyama anayefugwa ambayo inaashiriwa nalo. Kilichoko ni kwamba jamii ya wasemaji wa Kiswahili "imekubaliana" kutumia sauti-umbo "mbwa" kumrejelea mnyama huyo.

(b) *Ulinganuzi:* Ikiwa uhusiano baina ya kiashiria na kiashiriwa ni wa kinasibu, nivipi ambavyo alama hupata maana? Njia mojawapo imetajwa hapo juu, nayo ni "makuabaliano" miongoni mwa wasemaji lugha kuipa alama maana mahsusi. Lakini muhimu zaidi ni kwamba maana ya neon hutokana na tofauti yake na maneno mengine. Yaani neon hupewa maana ambayo inalitofautisha na maneno mengine katika mfumo wa lugha. Hivyo, maana ya neon "mbwa" inalitofautisha na "mbweha", "mbwiji", n.k. Sifa ya ulinganuzi wa alama za lugha inaelezeka vizuri zaidi kwa kutumia dhana ya ukinzaṇi uwiliuwili, ambapo maneno mawili yanayochukulika kama jozi yanajipambanua kama vinyume. Kwa mfano:

Mwanamume - mwnamke
Msichana - mvulana
Baba - mama

Sasa tuiangalie nadharia yenyewe ya upambanyaji. Hapa tutafafanua kwa

muhtasari vipengele vyake/vikuu. Neno "upambanyajii" aghalabu huchukuliwa kuwa ni kisawe cha "umuundoleo". Wale wanaopendelea kutumia neno la pili hufanya hivyo kwa kuzingatia ukweli kwamba nadharia tunayoizungumzia ni kama mwendelezo wa umundo. Wafuasi wa umuundo ndio ambao baadaye walikuja kubuni umuundoleo. Haya yalitokea baada ya wao kuona kuwa umuundo ulielekea kushindwa kujibu baadhi ya kile walichokiona kuwa ni maswali nyeti ya kifasihi yaliyozuka katika kipindi kinachohusika. Watu ambao mawazo yao yamejenga umuundoleo au uumbuaji kwa kiasi kikubwa ni Wafaransa. Nao ni mwanafalsafa/mwanafasihi Jacques Derrida, mwanahistoria Michel Foucault, na mhakiki Jacques lacan. Mwingine ni mtetezi wa ufeministi aitwaye Julia Kristeva.

Jacques Derrida alikuwa mfuasi wa umuundo lakini baadaye alianza kuikosoa nadharia hii. Alikuja kujitokeza kama mmojawapo wa wajenzi wakuu wa uumbuaji. Nadharia hii ilianza kuvuma katika nchi za ufaransa na Marekani katika kiaka ya sitini na sabini. Kanuni zake nyingi zilikinzana na umuundo. Kama mfano umuundo ulichukulia kazi ya kifasihi kuwa ni mfumo thabiti uliojengwa na elementi mahsusi. Derrida aliupindua mwelekeo huu akazua dhana ya mfululizo wa uashiriaji ambao hauna mwisho wala mipaka. Yaani kazi ya kifasihi sio mfumo funge wenye kitovu na mshikamano wa elementi bali ni kitu kisicho na uthabiti wa umbo. Aidha kazi ya kifasihi sio kitu ambacho chapaswa kupewa staha na kuhakikiwa kwa kufuata masharti na kanuni mahsusi. Badala yake kazi ya kifasihi inachukuliwa kama uwanja wa michezo. Mhakiki naye anachukuliwa kama mchazaji katika uwanja huo. Hivi ni kusema kuwa Derrida alijaribu kuubomoa uzito na unyeti wa fasihi na kuingiza ucheshi katika taratibu za uhakiki. Katika manzili haya, fasihi iliyopendelewa na wahakiki wa upambanyaji ni ile ya kiusasa ambayo haina umbo wala maana thabiti. Mfano hapa ni kazi mbili za Kezilahabi: *Nagona* na *Mazingile*. Kazi za aina hii ni mseto wa viashiria na misimbo ambavyo mhakiki anaweza kuvichezea apendavyo.

Lengo kuu la upambanyaji katika uhakiki ni kudhihirisha kwamba hakuna ushikamano wala uthabiti katika mifumo ya lugha na fasihi. Mhakiki anayeitumia nadharia hii hujaribu kuzipambanya matini za kifasihi, kuyabomoa machukulio yake na kuvivunjavunja vitovu vyake. Hata hivyo wafuasi wa upambanyaji wanadai kuwa uhakiki wao haudhamirii kuziangamiza kazi za kifasihi wala kuiangamiza fasihi. Akifafanua kanuni na malengo ya nadharia hii, mfuasi wake maarufu kutoka nchini Marekani

J.H. Miller (1976: 341), anasema kuwa "upambanjaji sio ubomoaji wa muundo wa matini bali ni kudhihirisha kwamba imejibomoa yenyewe. Msingi wake unaoonekana kuwa thabiti sio mwamba bali ni hewa nyepesi". Kwa maneno mengine kupambanya matini ni utaratibu wa kubainisha kwamba ndani mwake mna simulizi, maana na elementi nyingine nyingi ambazo zinakinzana.

Uchanganuzi wa matini ya kifasihi katika misingi ya upambanyaji hauangaliwi kama utafutaji wa maana iliyofichika, bali unachukuliwa kuwa ubainishaji wa mawezekano ya kimaana yasiyokuwa na maana wala kikomo. Hata dhana yenyewe ya matini pambanywa na inakuwa mwingilanomatini. Yaani katika hatua za uhakiki uchanganuzi unasambaa nje ya matini husika hadi kwenye matini zinazohusiana na kukaribiana nayo. Katika mkururo huu mipaka baina ya matini ya kifasihi na matini za aina nyingine inamomonyolewa. Fasihi inapokonywa hadi inayopewa katika uhakiki wa kijadi, ya kuwa na lugha ya kipekee ambayo ni ya kitamathali. Ndiposa upambanyaji unapendelea kuzitaja tungo za kifasihi kama matini ili kuziweka katika kiwango sawa na maandishi ya aina nyingine. Mtunzi wa kazi ya kifasihi naye anavuliwa hadhi yake. Uhakiki wa kiupambanyaji unampuuza mwandishi na kujikita tu katika kazi yake.

Mojawapo ya kaida muhimu za kimapokeo katika uhakiki na uandishi wa fasihi ni kwamba ukinzani unavunja kanuni za utunzi bora. Upambanyaji unajaribu kuivunja kanuni hii kwa kudai kwamba hakuna kazi ya kifasihi isiyokuwa na ukinzani katika viwango vya fani na dhamira. Lengo la nadharia hii ni kuibainisha mikinzano iliyomo katika kazi ya kifasihi. Kwa mujibu wa wafuasi wa nadharia hii mikinzano hiyo inathibitisha uajabu wa fasihi.

### 3. Upambanyaji Matini ya *Rosa Mistika*

Tahakiki hii imedhamiriwa kuonyesha jinsi upambanyaji unavyoweza kutumiwa katika uhakiki wa riwaya ya Kiswahili.

Kwa kifupi riwaya ya *Rosa Mistika* inashughulikia tatizo la malezi yasiyofaa na athari zake katika maisha ya wahusika. Tatizo la malezi mabaya linaleta madhara makubwa katika jamii. Wazo hili linajengwa kwa kutumia maisha ya Rosa ambayo yamejaa misukosuko na kuishia kwenye tanzia. Yote hayo yanatokana na upungufu wa malezi yake. Mwandishi anajaribu kuonyesha kwamba mfumo wa kimaadili wa jamii inayohusika unaelekea kuporomoka kutokana na tatizo lililotajwa hapo juu. Kwa kutumia nadharia ya

upambanyaji tutabainisha mikinzano iliyomo katika dhamira ya riwaya na pia katika machukulio ya mwandishi katika kuendeleza dhamira yake. Ukinzaniwili wenye nafasi kubwa katika matini ya *Rosa Mistika* na unaohusiana na dhamira ya malezi iliyotajwa hapo juu ni ule wa baba/mama. Hivi ni kusema kuwa katika familia na katika jamii kwa jumla baba ana nafasi yake na ana majukumu mahsusi katika malezi ya watoto. Mama naye vile vile. Mgawo huu wa wajibu wa baba kwa upande mmoja na mama kwa upande mwingine unajitokeza wazi wazi riwayani. Zakaria anapomtandika Rosa kwa "kosa" la kupata barua ya mapenzi kutoka kwa mwanafunzi mwenzake Charles Lusato, inaelezwa kuwa mzee huyo "hakufahamu kwamba kwa kumpiga bintiye alikuwa akiingilia utawala usio wake...." (uk.15). Yaani kazi ya kumnidhamisha Rosa sio ya baba. Maelezo mengine ambayo yanabainisha mgawo wa majukumu ya kimalezi baina ya baba na mama ni kama yafuatayo:

> Kama ni watoto wasichana, mara nyingi utakuta mama anajenga baba anabomoa; kama ni wavulana, baba anajenga mama anabomoa. Haya yote hutokea kwa kutofahamu wapi baba atawale zaidi na wapi mama (uk.56).

Mbali na kubainisha mgawo tunaouzungumzia, maelezo hayo pia yanaonyesha kwamba mgogoro wa kimalezi uliomo katika jamii inayohusika unatokana na wazazi kutotambua wajibu wao.

Sasa tuangalie jinsi mgawo wa majukumu ya kimalezi unavyojitokeza katika familia ya Zakaria. Ni nani—kati ya Zakaria na mkewe Regina—anayetekeleza wajibu wake na ni nani asiyeutekeleza? Ni nani wa kulaumiwa watoto kama Rosa wanapopata malezi mabaya? Majibu ya maswali haya yanapatikana kwa urahisi riwayani. Kwa upande mmoja kuna baba, yaani Zakaria ambaye ni mlevi na mjeuri. Ni mkali sana kwa binti zake na anawalinda ili wasiingiliane na wavulana. Hivyo, anawaharibu kwa kutowapa mwongozo ufaao. Kwa upande mwingine kuna mama, Regina, ambaye kitabia ni kinyume cha mumewe Zakaria. Yeye ni mpole, mvumilivu na anayewapenda watoto wake. Rosa anapoangamia hatimaye kutokana na malezi mahaya, mtu wa kulaumiwa ni Zakaria. Hii ndiyo hoja ambayo riwaya inajaribu kujenga.

Hata hivyo tunapozama zaidi katika matini ya riwaya, tunaona kuwa hoja hiyo haina msingi. Kwanza tuangalie mgawo wa wajibu wa kulea, yaani baba/mama. Ni kweli kwamba Zakaria ni mlevi na mapato yake nayafuja katika pombe. Inadokezwa kwamba wajibu wa baba katika hali kama ya Zakaria ambapo watoto wanaohusika ni wa kike (hasa Rosa na Flora ambao

ni wakubwa) ni kutimiza mahitaji yao kama malezi, chakula na ada za shule. Zakaria anashindwa kutimiza wajibu huu. Rosa anaposhinda katika mtihani wake na kupata nafasi kuendelea na masomo katika shule ya Rosary, Zakaria anashindwa kutoa pesa zinazohitajika. Inalazimu ng'ombe wa Regina auzwe ili kugharamia masomo ya Rosa. Pesa zinazopatikana Zakaria anaziiba na kwenda kuzifuja katika ulevi. Regina hakati tamaa. Anatengeneza pombe nyingi ya mihogo na kuuzia wanakijiji. Anapata pesa za kutosha kumwezesha Rosa kuendelea na masomo.

Baada ya matukio hayo matini inaelekea kusema kuwa hali isiyokuwa ya kawaida imetokea kwa kuwa mama amechukua wajibu wa baba. Ule mgawo wa wajibu baina ya baba na mama unaanza kumomonyoka. Sasa tuangalie wajibu wa mama. Katika ulimwengu wa riwayani, wajibu wa mama ni kuwapa ushauri watoto wa kike, hasa kuhusu mahusiano baina ya wanawake na wanaume. Je, Regina anawapa binti zake ushauri ufaao? Rosa anapokaribia kuondoka nyumbani kwenda shule ya bweni ya Rosary, mamake anamuonya:

> Jambo moja hasa ningependa kukuhadharisha; wavulana wakorofi. Huenda wakakutaka kwa mapenzi nia yao ikiwa tu kukupa mimba itakayokukatisha masomo yako. Daima wakwepe hao. Na kama utakuwa mpumbavu ukapata mimba usiitoe….. (uk.18).

Huo ndio ushauri ambao mama anampa bintiye ambaye anatoka nyumbani kwenda kukabiliana na ulimwengu mpya. Baada ya kifungu kirefu cha ushauri kama huo inaelezwa: "Regina alikuwa mwanamke mwenye busara ingawa hakuwa na kisomo chochote". Kwa hivyo inachukuliwa kuwa ushauri wake ni mzuri na wenye manufaa kwa Rosa. Lakini ni wazi kwamba hivyo si kweli. Maangamizi ya Rosa hatimaye yanatokana na kushindwa kwake kuingiliana ipasavyo na wanaume kwa kuwa hakuandaliwa vizuri kwa maingiliano kama hayo. Lawama kubwa anayostahili Zakaria ni kuwalinda binti zake kama wafungwa na kuwazuia kabisa kuingiliana na kuzoeana na wavulana. Ingetarajiwa kwamba mama angesaidia katika suala hili na kumfunza Rosa "mbinu" za kujenga mahusiano na wanaume na wakati huo huo kuhifadhi heshima na utu wake. Badala yake mama anampa ushauri wa kumpotosha, kama tulivyoona hapo juu. Hapa tunaona kuwa mama pia anashindwa kutekeleza wajibu wake. Katika hali kama hii ambapo wazazi wote wawili wanashindwa katika majukumu yao ya kulea watoto, mgawo wa wajibu baina ya mama kwa upande mmoja na baba kwa upande mwingine unakosa mantiki.

Hadithi ya Rosa imedhamiriwa kusawiri hali mbaya ya malezi katika jamii inayohusika. Kwa kuzingatia ukweli huu tunaona kuwa hakuna mantiki katika kumpa Rosa wazazi kama Regina na Zakaria ambao kwa mambo mengi ni watu wa kipekee. Sio wazazi wazuri katika muktadha wa riwayani. Tunachosema hapa ni kuwa hali ya kipekee kama ile ya Rosa na wazazi wake haiwezi kutumiwa kama kiwakilishi cha hali ilivyo kwa ujumla katika jamii. Matini ingekuwa na mantiki zaidi kama familia yenye malezi ya wastani ingetumiwa. Labda wasichana kama Thereza (rafikiye Rosa anapokuwa katika shule ya Rosary) walipata malezi ambayo ni afadhali kidogo. Hivi ni kwa sababu Thereza anapokuwa katika mazingira sawa na yale ya Rosa yeye anajimudu katika mahusiano yake na wanaume ilhali Rosa anatatizika sana. Lakini matini haitoi nafasi ya kulinganisha malezi ya Rosa na yale ya wasichana wengine wa rika lake. Hatuonyeshwi mazingira ya kifamilia ambapo wasichana kama Thereza walikulia. Matini inaeleza tu kwamba malezi ya Rosa ni ya kipekee kwa ubaya wake bila kutoa hata mfano mmoja wa malezi mazuri au ya kikawaida. Katika hali kama hii msomaji hapewi nafasi ya kuyatathmini malezi ya Rosa katika kazingira ya hali halisi ya jamii yake.

Tatizo jingine ni kuwa tangu mwanzo matini inajaribu kuonyesha kuwa hulka ya Rosa imejengwa na malezi yake. Suala la nafasi ya udhaifu wake binafsi halipewi nafasi. Linapachikwa tu mwishoni katika ndoto ya Emmanuel ambapo, mbele ya Mungu, Rosa anajitetea akidai kuwa tanzia ya maisha yake imetokana na babake; na Zakaria kwa upande wake akisema kuwa imetokana na ubaya na udhaifu wa Rosa. Hapa inabainika kuwa suala la mchango wa hulka ya Rosa katika tanzia ya maisha yake linaachwa nje kimakosa na ujanja wa kulipachika mwishoni unatumiwa. Ni ukweli dhahiri na wala sio jambo la mjadala kuwa maumbile ya mtu na malezi pamoja na mazingira yake kwa ujumla yanajenga tabia yake. Ukweli huu haushughulikiwi vya kutosha katika matini tunayoihakiki.

Tuangalie upande mwingine wa suala la malezi. Je, ni wazazi peke yao ambao wanahusika katika suala la malezi? Moja kwa moja jawabu ni la. Kwanza, kuna jamaa ambao wanatoa mchango muhimu katika malezi ya watoto. Ithibati zipo za kutosha kuonyesha kuwa katika jamii inayohusika riwayani, ujamaa uko hai. Kwa mfano Deogratias anapopeleka posa kwa Zakaria akitaka kumuoa Rosa, mzee huyo anamwambia: "Nitakutuma kwa jamaa zangu wote, pia kwa jamaa za mke wangu. Lazima ukawaombe mtoto, maana mtoto si wangu peke yangu" (uk.48). Ni ajabu kwamba mchango wa jamaa hao katika malezi ya Rosa haujitokezi riwayani. Ikiwa mtoto sio wa Zakaria peke yake, kwa nini jamaa zake hawakumsaidia

kumwongoa Rosa? Kwa nini hawajitokezi kumtilia Zakaria shinikizo ili aache kuwaharibu binti zake?
Pia kuna shule ambayo ni asasi muhimu sana katika malezi ya watoto. Ikumbukwe kwamba watoto wasomao shuleni hukaa huko kwa muda mrefu kuliko ule ambao wanakaa na wazazi wao, na hivyo athari za mazingira ya shuleni zimewasaidia wasichana wa rika la Rosa kujenga mahusiano ya kikawaida na wanaume. Mfano mzuri, kama ilivyotajwa hapo juu, ni Thereza. Inaelezwa kuwa Thereza hakuwa na mkururo wa marafiki wa kiume kama Rosa. Yeye alikuwa na wawili tu kwa kuwa "Alikuwa amekwisha jifunza mengi kuhusu wavulana". Alijifunza mwenyewe katika mazingira ya shuleni. Kwa nini Rosa hakujifunza hivyo? Kutokana na yote hayo, tunaona kuwa matini inakosa mantiki kwa kumlundikia Zakaria lawama kwa upotovu wa Rosa.

Kwa kumalizia, uchanganuzi wa matini ya *Rosa Mistika* katika misingi ya upambanyaji unadhihirisha kuwa nadharia hii ni chombo muafaka cha kuangazia mikinzano na mapengo ya mantiki katika masimulizi na maudhui ya riwaya hiyo.

**Marejeo**


Amuta, C. 1989. *The Theory of African Literature*. London: Zed Books.

Cinweizu, et al, 1985. *Toward the Decolonizatiaon of African Literature*. Enugu: Fourth Dinesion Publishers.

Culler, J. 1981. *The Pursuit of Signs: Semiotics, Literature and Deconstruction*. London: Routledge and Kegan Paul.

Derrida, J. 1976. *Of Grammatology* (Mtafsiri G. Spivak), John Hopkins University Press.

Eagleton; T. 1983. *Literary Theory: An Introduction*. Oxford: Blackwell Publishers.

Foucault, M. 1970. *The Order of Things*. London: Tavistock.

Kezilahabi, E. 1971. *Rosa Mistika*. Nairobi, Kenya Literature Bureau.

***Kiambatisho: Baadhi ya Istilahi Zilizotumiwa na Tafsiri Zake za Kiingereza***

| | | |
|---|---|---|
| **Alama** | - | sign |
| **Kiashiria** | - | signifier |
| **Kiashiriwa** | - | signified |
| **Kiusasa** | - | modernist |
| **Linganuzi** | - | differential |
| **Mfululizo wa uashiriaji** | - | chain of signification |
| **Nasibu** | - | arbitrary |
| **Ufeministi** | - | feminism |
| **Uhakiki mpya** | - | new criticism |
| **Ukinzani uwiliuwili** | - | binary opposition |
| **Umuundo** | - | structuralism |
| **Urasimu** | - | formalism |
| **Urasimu wa Kirusi** | | Russian formalism |
| **Upambanyaji** | - | deconstruction |